



وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَمْ يَكُنْ لَّهُ بِهِمْ حِلٌّ أَنْقَضُهُمْ لِمَنْ وَلَيْسَ لَهُمْ بِئْنَ يَمْلِكُوهُمْ أَنَّهُ
يَعْبُدُونِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

Jumapili, 1 Rabi' I 1447 H

24/08/2025 M

Na: HTS 1447 / 17

Taarifa kwa Vyombo vyaa Habari

Ujumbe kutoka Hizb ut Tahrir / Wilayah Sudan Waitembelea Idara ya Muongozo na Ushauri katika Jimbo la White Nile (Imetafsiriwa)

Ujumbe kutoka Hizb ut Tahrir / Wilayah Sudan – Mji wa Rabak, White Nile, uliitembelea Idara ya Muongozo na Ushauri mnamo Jumapili, 1 Rabi' al-Awwal 1447 H sawia na tarehe 24 Agosti 2025. Ujumbe huo ulikutana na mkuu wa Sekretarieti katika Jimbo la White Nile, Sheikh Abdul Mubara Mahmoud Al-Mahmoud. Ujumbe huo uliongozwa na Dkt. Ahmed Muhammad Fadl Al-Sayyid, mwanachama wa Hizb ut Tahrir, na alifuatana na Ustadh Faisal Madani, mwanachama wa Hizb ut Tahrir.

Baada ya kujitambulisha, mkuu wa ujumbe huo alieleza kuwa ziara hii inakuja ndani ya muundo wa kampeni iliyozinduliwa na Hizb ut Tahrir/Wilayah Sudan ya kuzuia kujitenga kwa Darfur, akiangazia hatari ya mpango huo kwa umoja wa nchi, ikizingatiwa kuwa ni suala la hatari ambalo lahitaji hatua za uhai au kifo.

Pia aliitaja kampeni iliyozinduliwa na hizb kutibua mpango wa kuitenga Sudan Kusini, akiashiria maafa na masaibu yaliyoikumba Sudan kutokana na kujitenga kwake, na jinsi Marekani ilivyofanikiwa katika hilo, na sasa inataka kuitenganisha Darfur.

Ujumbe huo pia ulijadili kuzingirwa kwa mji wa El Fasher na silaha ya njaa inayotumiwa dhidi ya watu wetu huko El Fasher, Deling, Kadugli na Gaza, ukitoa hadith za Mtume (saw) ambazo zinahimiza umoja baina ya Ummah.

Sheikh Abdul Mahmoud alikubaliana na kauli ya ujumbe huo na kusisitiza kuwa wanaunga mkuono umoja wa Ummah hata ikiwa itamaanisha kutumia silaha. Alisisitiza kwamba mimbari ziko wazi kwenu, na kwamba tutawaelekeza maimamu wa misikiti na wanachama wetu wote kuzungumzia kuhusu suala hili nyeti.

**Ibrahim Othman (Abu Khalil)
Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir
katika Wilayah Sudan**